

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



MWONGOZO WA USHAURI KWA WASAFIRI NA.17 WA TAREHE 19 MEI 2026 JUU YA TISHIO LA MLIPUKO WA EBOLA

Mnamo tarehe 15 Mei 2026, nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Jamhuri ya Uganda zilitangaza mlipuko wa ugonjwa wa Virusi vya Ebola (EVD). Kufuatia matamko haya, pamoja na tamko la Mganga mkuu wa serikali. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa ushauri na maelekezo kwa wasafiri juu ya hatua za kuchukua kukabiliana na tishio la ugonjwa huo. Ushauri huu unaenda sambamba na hatua zinazoendelea kutekelezwa kudhibiti mlipuko wa Mpox na Hantavirus kulingana na Kanuni za Afya za Kimataifa (2005) na Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka, 2009. Hivyo, kuanzia tarehe 19 Mei 2026 Serikali inaelekeza kutekeleza hatua zifuatazo;

1. Wasafiri wote wanaowasili nchini kutoka au kupitia DRC au Uganda wanatakiwa kujaza kwa uaminifu fomu ya ufuatiliaji wa hali ya afya za wasafiri katika mtandao kwa anuani ya <https://afyamsafiri.moh.go.tz>, kabla ya kuanza safari au fomu ya karatasi itakayotolewa kwenye vyombo vya usafiri au wakati wa kuwasili mpakani.
2. Katika kila mpaka (viwanja vya ndege, mipaka ya nchi kavu au bandari), wasafiri wote watapimwa joto la mwili na viashiria vingine vya kiafya na watakabainika watafanyiwa uchunguzi wa kina na Mamlaka za Afya Mipakani.
3. Wasafiri wote watapewa elimu ya afya juu ya namna ya kujikinga na ugonjwa huu na wanashauriwa kutoa taarifa katika kituo cha afya kilicho karibu au kupiga nambari ya simu **199 bila malipo** wanapoona au kujisikia dalili za ugonjwa wa Ebola au ugonjwa mwingine wowote wa kuambukiza.
4. Wasafiri na wafanyakazi wa vyombo vya usafiri wanapaswa kuzingatia hatua za kuzuia na kukinga maambukizi kama vile unawaji wa mikono kwa maji tiririka na sabuni, matumizi ya vitakasa mikono (sanitizers) na kuepuka msongamano.
5. Vyombo vya usafiri vitakavyohisiwa kuwa na maambukizi ya ugonjwa huu vitafanyiwa usibuaji na utakasaji (decontamination/disinfection) na Mamlaka za Afya Mipakani.

NB: Ushauri huu utapitiwa mara kwa mara kadri itakavyohitajika.

Handwritten signature of Dkt. Seif A. Shekalaghe in blue ink.

Dkt. Seif A. Shekalaghe
Katibu Mkuu
Wizara ya Afya